**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA**
**SHULE YA AWALI NA MSINGI MPANDA JUNIOR**

**Kumb. Na. FA/26/330/51/10** **29/12/2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA AJIRA YA MKATABA KATIKA SHULE YA AWALI NA MSINGI MPANDA JUNIOR PRE & PRIMARY SCHOOL (ENGLISH MEDIUM)

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda anawatangazia wananchi wote kuomba nafasi ya kazi ya ajira ya Mkataba kama ifuatavyo:

## 1. WALIMU (NAFASI 05)

- Mwalimu wa Hesabu (Mathematics) **Nafasi 02**
- Mwalimu wa Sayansi (Science) **Nafasi 01**
- Mwalimu wa masomo ya Geography, Art and Sports **nafasi 01**
- Mwalimu wa kusoma na kuandika (reading and writing) **nafasi 01**

### SIFA ZA WAOMBAJI

- Mwajiriwa anatakiwa awe na, Stashahada au Shahada katika Elimu ya Msingi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na uwezo wa kufundisha masomo kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa ufanisi.
- Mwenye uzoefu wa angalau miaka miwili ya ufundishaji atapewa kipaumbele.
- Awe na uwezo wa kuzungumza lugha mbili Kiswahili na kingereza kwa ufasaha.
- Awe amesomea somo husika.

### MAJUKUMU YA MWOMBAJI WA KAZI ZA UALIMU

- Kufundisha masomo atakayopangiwa kwa mujibu wa ratiba ya shule.
- Awe anazingatia haiba ya ualimu.
- Kuandaa na kutekeleza mipango ya ufundishaji na nyaraka zinazohusiana.
- Kudumisha nidhamu ya wanafunzi na mazingira chanya ya kujifunzia.
- Kushiriki kikamilifu katika shughuli na maendeleo ya shule.
- Kutunza na kutumia vizuri vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- Kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wa Shule kulingana na majukumu ya Shule .

**2. MPISHI (NAFASI 01)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na uwezo wa kuzungumza lugha mbili Kiswahili na kingereza kwa ufasaha
- Awe na maadili ya kitanzania
- Awe amemaliza kidato cha nne
- Awe mwenye uzoefu wa kufanya kazi za upishi

**MAJUKUMU YA MPISHI**

- Kuwapikia wanafunzi
- Kugawa chakula kwa wanafunzi
- Kuosha vyombo
- Kufanya usafi eneo la kazi
- Kufanya majukumu mengine atayopangiwa na mkuu wa shule

**3. WALEZI WA WATOTO (MATRONS) (NAFASI 02)**
**MAJUKUMU YA WALEZI WA WATOTO (MATRONS)**

- Kuwasimamia wanafunzi wakati wa kusafiri kutoka nyumbani kwenda shule na kutoka shule kurudi nyumbani baada ya masomo.
- Kusimamia nidhamu ya watoto kwenye gari wakati wa kwenda na kurudi shule.
- Kusimamia usafi wa gari linalotumika kusafirisha wanafunzi.
- Kutoa taarifa kwa mwalimu mkuu kuhusu usafirishaji wa wanafunzi
- Kuwasiliana na wazazi panapohitajika.
- Kufanya majukumu mengine atayopangiwa na mkuu wa shule

**MASHARTI YA JUMLA**

i) Waombaji wote wawasilishe barua za maombi ya kazi zilizoandikwa kwa mkono kwa lugha ya Kiingereza.

ii) Wawe ni Raia wa Tanzania umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

iii) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

iv) Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma vinavyohusiana na nafasi husika pamoja na nakala ya kitambulisho cha NIDA.

v) Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE)

**ZINGATIO;**

Barua zote za maombi ziletwe shule ya awali na Msingi **Mpanda Junior**.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **02/01/2026.**

Imetolewa na

MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA MPANDA
S.L.P. 216
MPANDA-KATAVI

Charles Ferdinand

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**